


# **TUKUTANE SOTE!**

## **LASST UNS BEGEGNEN!**

MWONGOZO WA MIKUTANO YA USHIRIKIANO YA VIJANA  
WA MAKANISA YA TANZANIA NA UJERUMANI –

KIRCHLICHE JUGENDBEGEGNUNGEN ZWISCHEN  
TANSANIA UND DEUTSCHLAND BEGLEITEN





Hiki ni kijitabu cha / Dies ist das Heft von:

---

## ***DIBAJI - IMPRESSUM***


M.R. Margarethe Reuter  
H.F. Helena Funk  
K.K. Kimata Kimatta  
F.B. Fred M. Bosire

Design: M.R. & H.F.  
Layout: M.R.  
Maps: H.F.

Created and printed: 2014  
eFeF (evangelisches Forum entwicklungspolitischer Freiwilligendienst)



# YALIYOMO - INHALT



<i>Utangulizi</i> – Vorwort	3
<i>Kozi ya lugha</i> – Kurzsprachkurs	5
<i>Habari kuhusu nchi na watu wake</i> – Länderinformationen	7
<i>Historia</i> – Geschichte	11
<i>Ibada</i> – Gottesdienst	13
<i>Misale ya Sala</i> – Gebete	15
<i>Nyimbo</i> – Lieder	17
<i>Heshima (na aibu)</i> – Höflichkeit (und Fettnäpfchen)	21
<i>Maoni yako ni muhimu!</i> – Deine Meinung ist gefragt!	23
<i>Ratiba yako</i> – Dein Programm	25
<i>Anwani na simu</i> – Kontakte	27
<i>Mambo yako</i> – Notizen	29

# UTANGULIZI

*Idadi ya mikutano ya vijana katika misingi ya kikanisa inazidi kukua. Mojawapo ya nchi zinazotembelewa zaidi kwa minajili ya mikutano hii ni Tanzania iliyo Mashariki ya Afrika.*

*Sisi wawili tuliorudi Ujerumani baada ya kufanya kazi za kujitolea huko Tanzania na shirika la weltwärts-Freiwilligen, tunaweza kusema kwamba mikutano hiyo ni kitu cha muhimu sana, na hili si tu katika kuimarisha kufahamiana na mahusiano ya muda mrefu, bali pia katika kuwezesha kufahamiana kati ya vijana. Hili ni muhimu sana kwa vijana kwani hata hapo baadaye basi watakuwa na haja ya kujihusisha na shughuli mbalimbali za kujitolea kutokana na uzeofu na changamoto walizozipata. Hata ingawa hivyo, tunahofia kuwa mara nyingi kuna upungufu wa matayarisho kimashauri kabla na baada ya kusafiri, na vile vile upungufu wa ushauri wakati vijana wangali ugenini. Upungufu huu unaweza kusababisha kukua kwa picha zisizo za kweli kuhusu jamii watakazozitembelea. Wakiwa kule ugenini, upungufu huu pamoja na ufupi wa wakati uliowekwa wa kukaa kule, mara nyingi hauwaruhusu au hautoi nafasi ya kutosha kujifunza na kupata picha zilizo sahihi, labda hata kuyakomaza mawazo yasiyo sahihi. Kwa hiyo, tukiyazingatia mafunzo tuliyapata tulipokuwa Tanzania, tunaona ni wito kwetu kuwapa moyo wanaojitayarisha kusafiri na kuwahamasisha hawa ndugu zetu wanaojitolea wawe na upeo mrefu katika shughuli hizi kuanzia nyumbani na mpaka ugenini.*

*Kijitabu hiki kamwe hakiwezi kutoa habari zote kuyahusu mambo na hali zinazoweza kutokea wakati wa kujumuika, lakini hata hivyo, tunaona ni muhimu kutoa vidokezo vya msingi kueleza jinsi ya kukutana na vile vile kutoa ushauri unaowajua wenzetu njia za kuwepo wakati na hata baada ya kukutana. Kwetu sisi ni jambo la muhimu kukiandika kijitabu hiki katika Kiswahili na Kijerumani ili kiweze kutumika pande zote mbili, yaani Tanzania na Ujerumani. Tungependa maandalizi yawe ya kuzingatia usawa katika nyanja zote husika, yaani kijamii na kisiasa. Kwa vile mikutano hii ni ya kidini, tumeona ni vyema kusiwe tu na habari kuhusu lugha na nchi, bali pia kuwe na habari za imani. Na haswa, ili habari za jamii ziandikike bila ya kufuata uvumi wala matukano, tumeamua kuwa na sehemu iulizayo „Maoni yako ni muhimu! – Deine Meinung ist gefragt!“ Sehemu ambayo itamhamasisha msomaji kuhusu matumizi ya lugha na habari potofu katika mazingira na katika lugha zetu. Kutoka hapa huenda msomaji atapata kipengele kimoja au kingine cha kuanzishia majadiliano au kuyatathmini maisha.*

*Hata kama kijitabu hiki hususan kimeandikwa kwa ajili ya mikutano ya vijana, habari zilizomo zinaweza pia kuwafaa watu wengine wanaosafiri, ndugu, jamaa na marafiki. Kama una maswali mengine unaweza kuwasiliana nasi:*

*helena.m.funk@gmail.com ama margarethe@familie-reuter.info.*

*Shukrani zetu za dhati ziwaendee marafiki walio Tanzania na walio Ujerumani waliotusaidia kwa hali na mali, kwa udi na uvumba na pia twashukuru toleo za eFeF kwa kututia moyo na kutupa mkono katika kukiandika hiki kijitabu. Tunawatakia kila la heri katika kukutana kwenu!*

*Wenu Helena na Margarethe*

# VORWORT



Jugendbegegnungen auf partnerschaftlicher Ebene finden im kirchlichen Kontext immer häufiger statt. Eines der am häufigsten bereisten Länder ist dabei Tansania in Ostafrika.

Uns – zwei zurückgekehrten weltwärts-Freiwilligen - fiel auf, dass Begegnungen ein sehr wichtiger Aspekt sind, um Partnerschaften langfristig zu stärken und, um sich gegenseitig kennenzulernen. Gerade auf der Ebene von jungen Erwachsenen kann dies ein sehr bestärkendes Element sein für zukünftiges Engagement.

Dennoch befürchten wir, dass es leider oftmals an einer ausreichenden Vor- und Nachbereitung sowie Begleitung mangelt. So besteht die Gefahr, dass durch den meist nur kurzzeitigen Aufenthalt im Partnerland stereotype Bilder verstärkt werden. Es ist uns ein Anliegen, mit den während des Auslandsjahres gesammelten Erfahrungen, die Motivation und Vorfreude auf die Begegnung zu stärken und auch dazu anzuregen, sich nachhaltig auf beiden Seiten – in den Heimatländern – zu engagieren.

Dieses Heft kann zwar keinesfalls alle Themenbereiche abdecken und für alle Situationen vorbereiten, die während der Begegnung auftreten können, jedoch möchten wir vor allem Akzente setzen, um zu sensibilisieren, und etwas an die Hand geben, was praktisch helfen und begleiten kann: vor, während und nach der Begegnung.

Außerdem war und ist es uns wichtig, das Heft zweisprachig zu gestalten, sodass es sowohl in Tansania als auch in Deutschland eingesetzt werden kann.

Wir wünschen uns eine politisch, sozial und gesellschaftlich relevante Vorbereitung und Begleitung gewährleisten zu können.

Da es sich um Jugendbegegnungen im kirchlichen Kontext handelt, ist es uns wichtig gewesen, dass neben Sprache und länderspezifischen Infos auch der gelebte Glaube nicht zu kurz kommt.

Um vor allem gesellschaftliche und soziale Themen vorurteilsfrei aufzugreifen, haben wir die Rubrik „*Maoni yako ni muhimu!* – Deine Meinung ist gefragt!“ mit ins Heft aufgenommen. Diese soll Anreize zu Diskussionen und dem kritischen Hinterfragen der eigenen Lebensgewohnheiten liefern.

Auch wenn sich das Heft in erster Linie an Jugendbegegnungen richtet, kann es gerne für weitere Partnerschaftsreisen und Delegationen sowie deren Angehörige verwendet werden.

Bei weiteren Fragen könnt Ihr Euch gerne bei uns melden:

*helena.m.funk@gmail.com* bzw. *margarethe@familie-reuter.info*

Unser besonderer Dank gilt allen Freunden, die uns sowohl in Tansania als auch in Deutschland mit Rat und Tat unterstützt haben sowie der eFeF-Reihe, die uns zu der Umsetzung der Idee inspirierte und Hilfestellung gegeben hat.

Alles Gute für Eure Begegnungen!

Eure Helena und Margarethe

# KOZI YA LUGHA

Frage	Swali	Antwort	Jibu
Hallo/ Hey	<i>Mambo</i>	Hallo/ Hey	<i>Poa</i>
Guten Morgen Guten Tag Guten Abend Gute Nacht	<i>Za asubuhi</i> <i>Za siku</i> <i>Za jioni</i> <i>Za usiku</i>	Guten Morgen Guten Mittag Guten Abend Gute Nacht	<i>Salama/Njema/</i> <i>Nzuri</i>
Auf Wiedersehen Bis bald Tschüss	<i>Tutaonana</i> <i>Baadaye</i> <i>Kwa heri</i>	Auf Wiedersehen Bis bald Tschüss	<i>Tutaonana</i> <i>Baadaye</i> <i>Kwa heri</i>
Wie geht's dir? Wie geht's euch?	<i>Hujambo?</i> <i>Hamjambo?</i>	(Mir geht's) gut. (uns geht's) gut	<i>Sijambo</i> <i>Hatujambo</i>
Wie war eure Reise? Wie war dein Tag gestern?	<i>Habari za safari?</i>  <i>Habari za jana?</i>	Gut	<i>Nzuri</i>
Wie heißt du? Wie heißen Sie? ( <i>kwa watu wazima</i> ) Und du?	<i>Unaitwa nani?</i>  <i>Na wewe je?</i>	Ich heiße...	<i>Naitwa...</i>
Wo kommst du her?	<i>Umetoka wapi?</i>	Ich komme aus Tansania	<i>Nimetoka Tanzania</i>
Wie alt bist du?	<i>Una miaka mingapi?</i>	Ich bin (achtzehn)Jahre alt	<i>Nina miaka (kumi na nane)</i>
Bitte	<i>Tafadhali/ karibu</i>	Danke	<i>Asante</i>
ja	<i>Ndiyo</i>		
nein	<i>Hapana</i>		
Entschuldigung	<i>Samahani</i>	Kein Problem	<i>Hamna shida</i>
Bitte langsamer/ nochmal	<i>Polepole tafadhali/</i> <i>Sema</i> <i>tena tafadhali</i>	Bitte auf Englisch	<i>Sema kwa</i> <i>Kiingereza tafadhali</i>
Was ist das?	<i>Hii ni nini?</i>	Was heißt das?	<i>Ina maana gani?/</i> <i>Inaitwa nini ?</i>
Was kostet das ?	<i>Hii ni bei gani ?</i>		



# KURZSPRACHKURS

<b>Swali</b>	<b>Frage</b>	<b>Jibu</b>	<b>Antwort</b>
<i>Shikamoo</i>	(Begrüßung gegenüber Älteren)	<i>Marahaba</i>	(Antwort des Älteren)
<i>Hujambo</i> <i>Hamjambo</i>	Wie geht's dir? Wie geht's euch?	<i>Sijambo</i> <i>Hatujambo</i>	Mir geht's gut Uns geht's gut
<i>Mambo vipi?</i>	Was geht? (Gleichaltrige)	<i>Poa/Safi/Salama</i>	Cool/Sauber/ Friedlich
<i>Habari</i> <i>-gani?</i> <i>-yako?</i> <i>-zenu?</i> <i>-za asubuhi/ mchana/jioni?</i> <i>-za safari?</i>	Nachricht -welche? -von dir? -von euch? -vom Morgen/ Mittag/Abend? -von der Reise?	<i>Nzuri</i> <i>Salama</i> <i>Njema</i>	Gut Friedlich Schön
<i>Hodi</i>	Anklopfen	<i>Karibu</i>	Willkommen
<i>Karibu</i> <i>Karibuni</i>	Willkommen (Du) (Ihr)	<i>Asante</i> <i>Asanteni</i>	Danke Dir Danke Euch
<i>Unaitwa nani?</i>	Wie heißt du?	<i>Naitwa ...</i>	Ich heiße...
<i>Na wewe je?</i>	Und du?	<i>Mimi ni...</i>	Ich bin...
<i>Umetoka wapi?</i>	Wo kommst du her?	<i>Nimetoka</i> <i>Ujerumani.</i>	Ich komme aus Deutschland
<i>Una miaka</i> <i>mingapi?</i>	Wie alt bist du?	<i>Nina miaka (kumi</i> <i>na nane)</i>	Ich bin (achtzehn) Jahre alt
<i>Kwa heri</i>	Auf Wiedersehen	<i>Tutaonana</i>	Wir werden uns wieder sehen
<i>Mchana mwema</i>	Guten Nachmittag	<i>Jioni njema</i>	Guten Abend
<i>Pole</i> <i>-na kazi</i> <i>-na safari</i>	Mein Mitgefühl -für deine Arbeit -für deine Reise	<i>Asante</i>	Danke
<i>Ndiyo</i>	Ja	<i>Hapana</i>	Nein
<i>Hii ni shilingi</i> <i>ngapi?</i>	Was kostet das?	<i>Hii ni nini?</i>	<i>Was ist das?</i>
<i>Sema kwa</i> <i>Kiingereza</i>	Sags auf Englisch	<i>Sema tena/taratibu</i>	Sags noch mal/langsam

# HABARI ZA NCHI NA WATU WAKE - TANZANIA

Tanzania ni nchi ambayo ipo mashariki ya Afrika kando ya Bahari ya Hindi. Upande wa kaskazini nchi jirani ni Kenya na Uganda, upande wa magharibi ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Burundi na upande wa kusini ni Zambia, Malawi na Msumbiji. Yanapatikana maziwa matatu makubwa: ziwa Victoria, ziwa Tanganyika na ziwa Nyasa. Toka zamani wamekuwa wakiishi watu wa jamii mbalimbali, wakiwemo Wabantu, Wanailoti na Wakushi. Kuanzia karne ya 700 au 800 wafanyabiashara kutoka Asia na Ulaya walifika pwani na athari za tamaduni zao zikaana kuingia Afrika Mashariki.

Baada ya bara la Afrika kugawa kati ya nchi za Ulaya mwaka 1884-85, utawala wa

kikoloni wa Ujerumani ulianza kutayarishwa na mwaka 1891 Tanganyika ilitawaliwa na Wajerumani. Mwaka 1920 baada ya Vita Vikuu vya Kwanza, utawala wa Tanganyika ulichukuliwa na Waingereza. Tanganyika ilipata Uhuru mwaka 1961 na mwaka 1964 Tanganyika iliungana na Zanzibar na kuitwa Tanzania (Kwa habari zaidi kuhusu Historia, tafadhali angalia sehemu inayoitwa "Historia – Geschichte").

Idadi ya watu Tanzania sasa ni takriban milioni 40.5. Lugha rasmi ya Tanzania ni Kiswahili, hata hivyo kuna jamii mbalimbali za watu wanaoongea lugha tofauti tofauti. Kiswahili kinazungumzwa rasmi Tanzania nzima. Mji mkuu wa Tanzania ni Dodoma, ulio katikati ya nchi. Mji mkubwa zaidi ni Dar es Salaam.

Hali ya hewa ni ya tropikali. Kuna kipindi cha mvua na kipindi cha kiangazi. Hata hivyo Tanzania ni nchi kubwa na kuna hali tofauti ya hewa katika sehemu tofauti. Kilimo ni sehemu muhimu zaidi katika uchumi wa nchi na kwa hiyo watu wengi wanategemea mapato ya kilimo. Kihistoria mfumo wa siasa wa awali ulikuza umoja na ushirikiano jambo ambalo bado linaonekana wazi na ni muhimu kwa wananchi.

Sarafu ya Tanzania inaitwa Shilingi (TSH /=) na Euro moja ni kama Shilingi elfu mbili. Tanzania kuna sehemu nyingi zenye biashara ya utalii ambazo zinatembelewa na wageni, kwa mfano: Mlima Kilimanjaro na mbuga ya wanyama ya Serengeti. Kila mwaka wageni wengi huja kutoka sehemu mbalimbali za dunia.

H.F., K.K., F.B.




## Wortschatz:

Land  
Einwohner\*innen  
Sprache  
Geld  
Tansania  
Deutschland  
Stadt



# INFORMATIONEN ZU LAND UND LEUTEN - TANSANIA



Tanzania

Tansania liegt in Ostafrika am Indischen Ozean. Im Norden grenzt es an die Länder Kenia und Uganda, im Westen an die Demokratische Republik Kongo, Ruanda und Burundi und im Süden an Sambia, Malawi und Mosambik. Tansania hat Zugang zu drei großen Seen: den Viktoriasee, den Lake Tanganyika und den Malawisee.

Seit jeher wurde es von verschiedenen Gruppen bewohnt, wie z.B. den Bantu, den Nailoti und den Kushiti. Ab dem 7. oder 8. Jahrhundert erreichten Händler\*innen aus Asien und Europa die Küste und begannen die Kultur in Ostafrika zu beeinflussen.

Nachdem der Kontinent Afrika unter den Ländern Europas aufgeteilt worden war (1884-1885), begann die deutsche Kolonialregierung ab

1891 Tanganyika zu regieren. Ab 1920, nach dem Zweiten Weltkrieg, wurde Tanganyika britische Kolonie. 1961 erhielt Tanganyika schließlich die Unabhängigkeit und vereinte sich 1964 mit Sansibar zu Tansania (Weitere Informationen zur Geschichte findest Du unter der Rubrik „Historia – Geschichte“).

Heute hat Tansania etwa 40.5 Mio Einwohner\*innen. Die offizielle National- und Amtssprache ist Kiswahili und wird im ganzen Land beherrscht, aber es gibt auch über 120 andere lokale Sprachen. Die Hauptstadt Tansanias ist Dodoma und befindet sich im geographischen Zentrum des Landes, jedoch ist Dar es Salaam die größere Stadt.

Das Klima ist tropisch mit Regen- und Trockenzeiten, aber wegen der Größe des Landes unterscheiden sich die Klimazonen in den verschiedenen Landesteilen.

Subsistenzwirtschaft nimmt einen großen Teil der Wirtschaft Tansanias ein, da viele Menschen von ihr abhängen. Bis heute ist der Zusammenhalt ein wichtiges Charakteristikum der Gesellschaft, es wird sich gegenseitig viel geholfen.

Die Währung in Tansania heißt „Schilling“ (TSH /=). Ein Euro entspricht ungefähr 2000 Tansanischen Schillingen.

Es gibt eine Menge Sehenswürdigkeiten im ganzen Land, z.B. den Kilimanjaro und den Serengeti-Nationalpark, die jedes Jahr viele Touristen aus der ganzen Welt anziehen.

H.F., K.K., M.R.

## **Msamiati:**

*nchi*  
*wananchi*  
*lugha*  
*pesa*  
*Tanzania*  
*Ujerumani*  
*mji*

# HABARI ZA NCHI NA WATU WAKE - UJERUMANI

Ujerumani ni nchi iliyo katikati ya Ulaya. Kusini mwa Ujerumani kuna milima ya Alps na kaskazini ya Ujerumani kuna Bahari ya Kaskazini na Bahari ya Baltik. pia kuna mito mingi mikubwa.

Lugha ya Ujerumani ni Kijerumani, ambacho kina lahaja mbalimbali. Tofauti na Tanzania, hakuna lugha nyingi za asili kama ilivyo Tanzania. Ujerumani ina wananchi takriban milioni 82. Mji mkuu ni Berlin na nchi ina majimbo 16. Ujerumani ni nchi mwanachama wa Jamuiya ya Ulaya.

Ujerumani ni taifa changa kidogo yaani baada ya Vita Vikuu vya Pili iligawa kuwa nchi mbili. Tangu 1990 nchi hizi ziliungana tena na kuwa moja (Kwa habari zaidi kuhusu Historia, tafadhali angalia sehemu inayoitwa "Historia – Geschichte").

Uti wa uchumi wa Ujerumani ni viwanda hasa vya magari na vifaa mbalimbali vya teknolojia. Ujerumani ina mfumo madhubuti wa kijamii ambao unawalazimu wanachi wake wote wawe na bima ya afya, ya ajira na ya malipo ya uzeeni. Kwa sababu hizi Wajerumani wanalazimika kulipa kodi kubwa kutoka kwa mapato yao ili kugharamia bima hizo.

Hali ya hewa inaambatana na vipindi vya mwaka. Kuna majira ya baridi kuu, baridi, mvua ama jua kali. Wakati wa majira ya baridi kuu (mwezi wa kumi na moja hadi mwezi wa pili) mara nyingi kuna theluji na wakati mwingine majira ya joto (mwezi wa sita hadi mwezi wa nane) inawezekana kuwa na jua kali na joto karibia kama Dar es Salaam.

Kuanzia mwaka 2000 Wajerumani wanatumia sarafu ya Euro € (tamka „yuro“).



Kuna sehemu nyingi za kihistoria Ujerumani: Kuna majengo ya kasri na makanisa ambayo yalijengwa hata zaidi ya miaka mia sita iliyopita.

K.K., H.F., F.B.

## Wortschatz:

Norden  
Süden  
Osten  
Westen  
Meer  
Klima

## INFORMATIONEN ZU LAND UND LEUTEN - DEUTSCHLAND

Deutschland ist ein Land in Mitteleuropa. Im Süden liegen die Alpen und im Norden liegt Deutschland an der Nord- und Ostsee. Außerdem gibt es viele große Flüsse.

Die Landessprache ist Deutsch, zwar gibt es verschiedene regionale Dialekte, jedoch keine verschiedenen Sprachen wie in Tansania.

Deutschland hat ca. 82 Mio Einwohner\*innen

Die Hauptstadt ist Berlin und Deutschland ist in 16 Bundesländer organisiert.

Deutschland gehört zur Europäischen Union.

Es ist eine recht „junge“ Nation, da sie nach dem Zweiten Weltkrieg zwei geteilt wurde. Seit 1990 ist der Staat wiedervereint. (Weitere Informationen zur Geschichte findest Du unter der Rubrik „Historia – Geschichte“)

Die wirtschaftliche Stärke liegt vor allem im Export von Technik und Autos.

Außerdem hat die Bundesrepublik Deutschland ein recht starkes Sozialsystem mit Krankenversicherung und Arbeitslosengeld. Diese Ausgaben können unter anderem nur durch die relativ hohen Steuerzahlungen der Bürger\*innen finanziert werden.

Das Wetter ist je nach Jahreszeit warm, nass, oder kalt. Im Winter (November bis Februar) liegt oft Schnee und im Sommer (Juni bis August) kann es heiß werden, fast wie in Dar es Salaam.

Gezahlt wird in Deutschland seit dem Jahr 2000 mit dem Euro.

In Deutschland gibt es viele geschichtsträchtige Plätze und Gebäude: So zum Beispiel Burgen, Kirchen und Schlösser, die vor mehr als 600 Jahren gebaut wurden.

H.F., M.R.



### **Msamiati:**

*kaskazini*

*kusini*

*mashariki*

*magharibi*

*bahari*

*hali ya hewa*

# HISTORIA - GESCHICHTE

*Ishara* – Legende:

Tanzania

Deutschland

Tanzania & Deutschland

*Walikuja Waarabu, biashara na wakazi wa pwani ikaanza* - Ansiedlung von AraberInnen, Aufbau eines Handelsnetzwerkes

*Utawala wa Kireno Zanzibar* - Portugiesische Herrschaft auf Sansibar

*Tawala za Ujerumani* - Deutscher Bund

*Mkutano wa Berlin: Tanganyika ikawa koloni ya Ujerumani*  
Berliner Konferenz: Deutschland wird Kolonialmacht über Tanganyika

*Jamhuri ya Weimar, Demokrasia ya bunge* - Weimarer Republik, parlamentarische Demokratie

*Mapinduzi ya Machi Ujerumani* - „Märzrevolution“

*Vita Vikuu vya Kwanza* - Erster Weltkrieg

~800-1500

1500-1699

1815-66

1848/49

1884

1914-18

1918-33

~1000-1806

1517

1699

1844

1871-1918

1890

1897

1905-07

1919

*Martin Luther atangaza tasnifu 95 zilizotenganisha dini ya Kikristu*

95 Thesen von Martin Luther, Spaltung des Christentums

*Dola takatifu la kirumi serikali ya Kaisari Askovu wa kanisa Katoliki* - Heiliges Römisches Reich Deutscher Nationen unter kaiserlicher und päpstlicher Herrschaft

*Dola la Kaisari chini ya katiba ya Bismarck* - Deutsches Kaiserreich unter Bismarckischer Reichsverfassung

*Wamissionari wa Kwanza wafika Africa Mashariki* - Erste Missionare in Ostafrika

*Waarabu kutoka Oman wawafukuza Wareno* - Vertreibung der Portugiesen durch Omanis


*Uingireza ilichukua wadhifa ya kuilinda Zanzibar* - Sansibar wird britisches Protektorat

*Vita vya Majimaji* - Majiji-Krieg

*Mwisho wa Biashara ya Utumwa* - Abschaffung des Sklavenhandels

*Makubaliano ya Versailles: Uingireza ilipata mamlaka Kuitawala Tanganyika* - Versailler Vertrag: Großbritannien erhält Administrationsmandat über Tanganyika









# IBADA

## *Baba Yetu*

*Baba yetu uliye mbinguni,  
Jina lako litukuzwe,  
Ufalme wako uje,  
Mapenzi yako yatimizwe  
hapa duniani kama huko mbinguni.  
Utupe leo riziki yetu,  
Utusamehe makosa yetu,  
kama sisi tunavyowasamehe  
waliotukosea.  
Usitutie majaribuni,  
lakini utuokoe na yule muovu.  
Kwa kuwa ufalme ni wako,  
na nguvu na utukufu  
hata milele.  
Amina.*

## *Imani ya Mituma*

*Namwamini Mungu, Baba Mwenyezi, Muumba wa mbingu na dunia;*

*Namwamini Yesu Kristo, Mwana wake wa pekee, Bwana wetu,  
aliyechukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu,  
akazaliwa na Bikira Maria.*

*Akateswa kwa mamlaka ya Ponsio Pilato,  
akasulibiwa, akafa, akazikwa,  
akashuka kuzimuni siku ya tatu akafufuka kutoka kwa wafu,  
akapaa mbinguni,  
ameketi kuume kwa Mungu Baba Mwenyezi,  
kutoka huko atakuja  
kuwahukumu walio hai na wafu.*

*Namwamini Roho Mtakatifu:  
Kanisa takatifu la Kristo lililo moja tu,  
ushirika wa watakatifu,  
ondoleo la dhambi,  
kufufuliwa kwa miili,  
na uzima wa milele.  
Amina.*

## *Neema (2 Wakorintho 13:13)*

*Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo,  
na upendo wa Mungu Baba,  
na ushirika wa Roho Mtakatifu  
ukae nasi sote,  
sasa na hata milele.  
Amina.*

## *Baraka (Hesabu 6, 24-26)*

*Bwana akubariki, na kukulinda;  
Bwana akuangazie nuru za uso wake,  
na kukufadhili;  
Bwana akuinulie uso wake,  
na kukupa amani.*

# GOTTESDIENST



## Das Vaterunser

Vater unser im Himmel  
Geheiligt werde dein Name.  
Dein Reich komme.  
Dein Wille geschehe,  
wie im Himmel, so auf Erden.  
Unser tägliches Brot gib uns heute.  
Und vergib uns unsere Schuld,  
wie auch wir vergeben unsern  
Schuldigern.  
Und führe uns nicht in Versuchung,  
sondern erlöse uns von dem Bösen.  
Denn dein ist das Reich  
und die Kraft und die Herrlichkeit  
in Ewigkeit.  
Amen.

## Das apostolische Glaubensbekenntnis


Ich glaube an Gott, den Vater, den Allmächtigen,  
den Schöpfer des Himmels und der Erde.  
Und an Jesus Christus, seinen eingeborenen Sohn, unsern Herrn,  
empfangen durch den Heiligen Geist, geboren von der Jungfrau Maria,  
gelitten unter Pontius Pilatus,  
gekreuzigt, gestorben und begraben,  
hinabgestiegen in das Reich des Todes,  
am dritten Tage auferstanden von den Toten,  
aufgefahren in den Himmel;  
er sitzt zur Rechten Gottes, des allmächtigen Vaters;  
von dort wird er kommen, zu richten die Lebenden und die Toten.  
Ich glaube an den Heiligen Geist,  
die heilige christliche Kirche,  
Gemeinschaft der Heiligen,  
Vergebung der Sünden,  
Auferstehung der Toten  
und das ewige Leben.  
Amen.

## Gnade-Gebet (nach 2. Korinther 13;13)

Die Gnade unseres Herrn Jesus Christus  
und die Liebe Gottes  
und die Gemeinschaft des Heiligen  
Geistes sei mit uns allen,  
jetzt und in Ewigkeit.  
Amen.

## Segensspruch (4. Mose 6, 24-26)

Der Herr segne dich und behüte dich;  
der Herr lasse sein Angesicht leuchten  
über dir und sei dir gnädig;  
der Herr hebe sein Angesicht über dich  
und gebe dir Frieden.



# MISALE YA SALA

## *Sala kabla ya kula*

*Njoo kwetu Bwana Yesu,  
uwe mgeni wetu  
ubariki chakula hiki kilichotoka  
mikononi mwako.  
Amina.*

## *Sala kabla ya kulala*

*Nimechoka, naenda kulala,  
nafunga macho yangu mawili,  
baba, niangaze  
ninapolala.  
Amina.*

*Utafsiri: H.F.*

## **Zaburi 23**

*Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu.  
Katika malisho ya majani mabichi hunilaza,  
kando ya maji ya utulivu huniongoza.  
Hunihusisha nafsi yangu;  
na kuniongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake.  
Naam, ninapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti,  
sitaogopa mabaya; kwa maana wewe upo pamoja nami,  
gongo lako na fimbo yako vyanifariji.  
Waandaa meza mbele yangu, machoni pa watesi wangu.  
Umenipaka mafuta kichwani pangu,  
na kikombe changu kinafurika.  
Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu,  
nami nitakaa nyumbani mwa Bwana milele.*

### **Wortschatz:**

Pastor(in)/Pfarrer(in)  
Kirche  
Gottesdienst  
Gebet  
beten  
Kollekte  
Lied  
singen  
Chor  
Abendmahl  
Evangelist(in)  
Abkündigung

# GEBETE



## Tischgebet

Komm Herr Jesus,  
sei unser Gast  
und segne,  
was du uns beschert hast.  
Amen.

## Nachtgebet

Müde bin ich, geh' zur Ruh',  
schließe beide Äuglein zu.  
Vater, laß die Augen dein  
über meinem Bette sein.  
Amen.

## Psalm 23

Der Herr ist mein Hirte; mir wird nichts mangeln.  
Er weidet mich auf grüner Aue und  
führet mich zum frischen Wasser  
Er erquicket meine Seele;  
er führet mich auf rechter Straße um seines Namens willen.  
Und ob ich schon wanderte im finstern Tal,  
fürchte ich kein Unglück;  
denn du bist bei mir, dein Stecken und dein Stab trösten mich.  
Du bereitest vor mir einen Tisch im Angesicht meiner Feinde.  
Du salbest mein Haupt mit Öl  
und schenkest mir voll ein.  
Gutes und Barmherzigkeit werden mir folgen mein Leben lang,  
und ich werde bleiben im Hause des Herrn immerdar.

### ***Msamiati:***

*Mchungaji*

*kanisa*

*ibada*

*sala*

*kuomba*

*sadaka*

*wimbo*


*kuimba*

*kwaya*

*Meza ya Bwana*

*Mwinjilisti*

*tangazo*



# NYIMBO - LIEDER

## Mungu Ni Pendo



Mun - gu ni pen - do a - pen - da wa - tu, Mung - gu ni pen - do a - ni - pen - da.

Si - ki - li - ze - ni fu - ra - ha yan - gu Mun - gu ni pen - do a - ni - pen - da.

2. *Nilipotea katika dhambi  
Nikawa mtumwa wa shetani.  
Chorus: Sikilizeni furaha yangu...*

3. *Akaja Yesu kunikomboa,  
Yeye kanipa kuwa huru.  
Sikilizeni furaha yangu...*

4. *Sababu hii namtumikia,  
Namsifu Yeye Siku zote.  
Sikilizeni furaha yangu...*

1. Gott ist die Liebe,  
lässt mich erlösen,  
Gott ist die Liebe, Er liebt auch mich.

Refrain: Drum sag ich's noch einmal:  
Gott ist die Liebe! Gott ist die Liebe,  
Er liebt auch mich.

2. Ich lag in Banden der bösen Sünde,  
ich lag in Banden und konnt' nicht los.  
Drum sag ich's noch einmal:...

3. Er sandte Jesus, den treuen Heiland,  
Er sandte Jesus und macht mich los.  
Drum sag ich's noch einmal:...

4. Dich will ich preisen, Du ewge Liebe,  
Dich will ich loben, solange ich bin.  
Drum sag ich's noch einmal:...



# Möge die Straße uns zusammenführen - Njia zetu zikutane tena

Chords: F, C, Dm, Am, B, F, C, C7

Voice: Mö - ge die Sta - ße uns zu - sam - men - füh - ren und der Wind in dei - nem Rü - cken sein;  
N - ji - a ze - tu zi - ku - ta - ne te - na na - si tu - ku - ta - ne nji - a - ni;

5. Vo.: sanft fal - le Re - gen auf dei - ne Fel - der und warm auf dein Ge - sicht der Son - nen -  
mvu - a ya kia - si in - ye - she masha - mba - ni Ju - a ling' - a - re pa - ko uso -  
F B Am F C7 F G7 C C7

8. Vo.: schein. Und bis wir uns wie - der - se - hen hal - te Gott dich fest in sei - ner Hand.  
ni m - pa - ka tu - taka - poo - na - na a - ku - shi - ke Mu - ngu mko - no - ni  
F C Dm Am B C7 F

13. Vo.: Und bis wir uns wie - der - se - hen hal - te Gott dich fest in sei - ner Hand.  
na mpa - ka tu - ta - ka - po - o - na - na a - ku - shi - ke Mu - ngu mko - no - ni.

2. Führe die Straße, die du gehst,  
immer nur zu deinem Ziel bergab;  
hab', wenn es kühl wird, warme  
Gedanken und den vollen Mond  
in dunkler Nacht.

Refrain: Und bis wir uns wiedersehen...

3. Bis wir uns mal wiedersehen, hoffe  
ich, dass Gott dich nicht verlässt;  
er halte dich in seinen Händen, doch  
drücke seine Faust dich nicht zu fest.

Und bis wir uns wiedersehen...

2. Njia upitazo daima zikuongoze  
kufikia malengo. Ikija baridi uwe na  
wazo moto, mbalamwezi i'gizani.

Chorus: Mpaka tutakapoonana...

3. Na mpaka tutakapoonana, naomba  
Mungu asikuache, akushike mkono  
lakini kamwe mkono wake usikuponde.

Mpaka tutakapoonana...

(Utafsiri: K.K., H.F., M.R.)

# Hakuna Mungu kama wewe - Es gibt keinen Gott wie dich

Voice

Ha - ku - na Mu - ngu ka - ma we - we ha - ku - na Mu - ngu ka - ma we - we ha -  
Es gibt kein - en Go - tt wie di - ch es gibt kein - en Go - tt wie di - ch es

Vo.

ku - na Mu - ngu ka - ma we - we ha - ku - na ha - ta - ku - we - po ni -  
gibt kein - nen Go - tt wie di - ch es gibt wirk - lich kein - nen wie dich ich

Vo.

me - tem - be - a ko - te ko - te ni - me - zun - gu - ka ko - te ko - te ni -  
bi - n sch - on vi - el ge - rei - st, scho - n vi - el he - rum ge - kom - men, ich

Vo.

me - ta - fu - ta ko - te ko - te ha - ku - na ha - ta - ku - we - po  
ha - be üb - ber - all ge - such - t, es gi - bt wirk - lich kein - en wie dich

## Shona:

(Übersetzung: H.F.)

*Hakuna wakaita saJesu  
Hakuna wakaita saye  
Hakuna wakaita saJesu  
Haku- Hakuna  
Ndamhanya mhanya pose pose  
Ndatenderera pose pose  
Ndatsvaka tsvaka pose pose  
Haku-Hakuna*

## English

*There's no one there's no one like Jesus  
There's no one there's no one like him  
There's no one there's no one like Jesus  
There's no one there's no one like him  
I walked, I walked, no one, no one  
I turned around, no one, no one  
I searched, I searched, no one, no one  
There's no one there's no one like him*

## Français

*Il n' y a vraiment personne comme Jésus  
Il n' y a vraiment personne comme Jésus  
Il n' y a vraiment personne comme Jésus  
Il n' y a vraiment personne comme lui  
Je marche, marche, personne, personne  
Je tourne, tourne, personne, personne  
Je fouille, fouille, personne, personne  
Il n' y a vraiment personne comme lui.*

# Laudate omnes gentes



Voice

Lau - da - te om - nes gen - tes, lau - da - te Do - mi -  
 Si - fu - ni wa - tu wo - te, si - fu - ni Mwen - ye -  
 Lob - singt, ihr Völ - ker al - le, lob - singt und preist den  
 Sing prai - ses, all you peo - ples, sing prai - ses to the

Vo. <sup>4</sup>

num. Lau - da - te om - nes gen - tes, lau - da - te Do - mi -  
 zi. Si - fu - ni wa - tu wo - te, si - fu - ni Mwen - ye -  
 Herrn. Lob - singt ihr Völ - ker al - le, lob - singt und preist den  
 Lord. Sing prai - ses, all you peo - ples, sing prai - ses to the

Vo. <sup>8</sup>

num. Lau  
 zi. Si  
 Herrn. Lob  
 Lord. Sing

# Neno litasimama

Voice


Ne - no li - ta - si - ma - ma Ne - no li - ta - si - ma - ma

Vo. <sup>5</sup>

Ma - mbo yo - te ya - ta - pi - ta la - ki - ni ne - no li - ta - si - ma - ma

Das Wort wird bestehen bleiben, das Wort wird bestehen bleiben,  
 alles wird vorübergehen, aber das Wort wird bestehen bleiben.

(Übersetzung: M.R.)



# HESHIMA (NA AIBU)

## *Ujerumani ... –* In Deutschland ...

*... ni vizuri kufunga kinywa wakati wa kitafuna chakula –*  
... ist es höflich, den Mund beim Kauen zu schließen

*... mara nyingine ni muhimu kumwuliza mwenyeji wako kama utaweza kuchukua kitu, kama vile chakula, hata kama kipo kingi –*  
... ist es manchmal wichtig die „Hausmutter“ zu fragen, bevor man sich etwas nimmt, z.B. Essen, auch wenn mehr als genug davon da ist

*...kuna mapipa mengi ya takataka tofauti: karatasi, plastiki, mabaki ya chakula, chupa na kadhalika zinatengwa na kutupwa katika pipa tofauti n.k. –*  
... gibt es viele Mülleimer, für Papier-, Plastik-, Kompost- und Restmüll u.s.w.

*... si vizuri hata kidogo kumwambia mtu eti amenenepa: ni matukano na wala si sifa –*  
... ist es überhaupt nicht gut, einem Menschen zu sagen, dass er oder sie zugenommen hat

*... ni kawaida kuwaaga wageni mlangoni bila ya kuwasindikiza nje –*  
... ist es normal Gäste an der Haustür zu verabschieden

*...ni heshima kutochelewa; kama haikuepukika na umechelewa sana; kumjulisha anayekusubiri kwamba utachelewa ni muhimu –*  
... ist es höflich pünktlich zu sein oder den Wartenden bei Verspätung zu informieren

*...kwa kawaida unasubiri wakati taa ya trafiki ni nyekundu –*  
...ist es gesetzlich vorgeschrieben, zu warten, wenn die Ampel rot ist

...

### Wortschatz:

diskutieren  
Vorurteil  
Respekt  
Peinlichkeit  
Verhalten  
er/sie/es ist gut..  
er/sie/es ist schlecht

# HÖFLICHKEIT (UND FETTNÄPFCHEN)

## Tanzania... - In Tansania ...

...*mara nyingi si vizuri kukataa ukikaribishwa (kwa chakula, vinywaji, n.k.) ni bora kula kidogo au kutoa sababu nzuri -*

...ist es oft nicht höflich eine Einladung (zum Essen, Trinken etc.) auszuschlagen, es ist besser zumindest ein bisschen zu essen oder einen triftigen Grund zu nennen

...*ukimpa mtu kitu chochote au ukipokea kitu chochote kutoka kwa mtu tumia mkono wa kulia -*

...wenn du jemanden etwas gibst's oder etwas annimmst, benutze die rechte Hand

...*ni kitu cha heshima kuwa na wakati wa kusalimiana hasa vijijini, na wazee au na majirani... -*

...ist es vor allem auf dem Land eine Sache der Höflichkeit, sich die Zeit zu nehmen, zu grüßen, vor allem Ältere, Nachbarn...

... *mara nyingi ni pongezi kumwambia mtu, kwamba amenenepa, lakini si vizuri hata kidogo kumwambia mtu kwamba amekonda -*

... ist es meistens ein Kompliment, jemandem zu sagen, dass er oder sie wohlgenährt ist (=gut gehen) aber es ist nicht gut, jemandem zu sagen, dass er oder sie abgenommen hat

...*kuna mipaka ya mambo ya mapenzi ambayo hairuhusiwi kuivuka hadharani (kwa mfano kumbusu au kumpapasapapasa mtu) -*

...gibt es Grenzen, Zuneigung in der Öffentlichkeit zu zeigen, die nicht überschritten werden dürfen (z.B. jemanden zu küssen oder sich anzufassen)

### Msamiati:

kujadili  
chuki  
heshima  
aibu  
tabia  
ni nzuri  
ni mbaya

... *ni heshima kumsindikiza mgeni wako kidogo na kumsaidia kubeba mizigo yake -*

... ist es höflich seine Gäste zu begleiten und ihnen beim Tragen des Gepäcks zu helfen

...



## MAONI YAKO NI MUHIMU! - DEINE MEINUNG IST GEFRAGT!

*Jiulizeni kama ni kweli na jadianeni mambo yalivyo nyumbani kwenu. Ni muhimu kujadili ili tusikuze chuki au picha potofu!*

Fragt Euch, ob die Aussagen wahr sind und diskutiert gemeinsam, wie es bei Euch zuhause gehandhabt wird. Es ist wichtig, darüber zu diskutieren, damit wir keine Vorurteile schaffen!

*„Je, ni vigumu kupata elimu ya juu kwa sababu ni ghali, ungependa kuwa na madaliko gani? -*

Es ist schwierig höhere Bildung zu bekommen, denn die Ausbildung ist teuer. Was könnten mögliche Veränderungen sein?“

*„Wakati una maana gani kwako na maishani mwako? -*

Welche Bedeutung hat Zeit für dich und dein Leben?“

*„Je, wewe unaionaje 'misaada ya maendeleo' ? Ni muhimu na endelevu? -*

Wie siehst du es? Ist 'Entwicklungshilfe' sinnvoll und nachhaltig?“

*„Je, jamii na serekali inawasaidiaje watu walio katika hali ngumu, kama vile wazee, watu wasio na kazi, watu wasiojiweza, wagonjwa...? -*

Wie kümmert sich die Gemeinschaft und der Staat um Menschen in schwierigen Situationen, wie Alte, Arbeitslose, Menschen mit Behinderung, Kranke...?“

*„Familia ni nani? - Wer sind Verwandte?“*

*„Wewe unafikiri nini? Nchi yako ni nchi ya amani? - Was denkst du? Ist dein Land ein friedliches Land?“*

*„Uhifadhi wa mazingira una umuhimu gani kwako? - Was bedeutet Umweltschutz für dich?“*

*„Je, ni nguo gani zinazofaa kuvaliwa nyumbani/shuleni/kanisani na wanawake/ na wanaume? - Welche Art von Kleidung ist für Männer und welche ist für Frauen passend, für Zuhause/für die Schule/für die Kirche?“*

„Mtoto mzuri ni mtoto yupi? -  
Was macht ein gutes Kind aus?“

„Ulisaidia kufanya kazi gani  
nyumbani utotoni -  
Wo hast du bei euch Zuhause  
mitgeholfen, als du klein warst?“

„Nitapata adhabu gani  
nikifanya kosa? -  
Was für eine Strafe  
bekomme ich, wenn ich  
einen Fehler mache?“

„Kuwa mwaminifu na kuwa na mpenzi mmoja kwa wakati moja  
au mpenzi moja maishani zina maana gani katika maisha yako?  
- Sich treu zu sein und eine Liebe fürs Leben zu haben. Welche  
Bedeutung hat dies in deinem Leben?“

„Je katika imani yako Mungu  
Mwenyezi ana maana gani na je  
shetani ana maana gani? -  
Welche Bedeutung hat der  
Allmächtige Gott und welche  
Bedeutung hat der Teufel in  
deinem Glauben?“

„Je, wanawake na wanaume  
wana haki sawa? -  
Haben Frauen und Männer die  
gleichen Rechte?“

„Imani ina maana gani katika  
maisha yako? -  
Welche Bedeutung hat der  
Glaube in deinem Leben?“

„Unapatwa na fikira gani unapomwona mtu asiye Mwafrika Tanzania? Au  
ukimwona mtu asiye Mzungu Ujerumani? (Unajitambulisha vipi na rangi ya  
ngozi (binafsi na kitaifa)?) -  
Welche Bedeutung hat die Hautfarbe für dich für deine (National- oder  
Selbst-)Identität? (Welche Idee kommt dir zum Beispiel, wenn du einem  
'Nicht-Afrikanisch-Aussehenden' Menschen in Tansania, oder einem 'Nicht-  
Europäisch-Aussehenden' Menschen in Deutschland begegnest, sind das  
deswegen keine Tansanier\*innen und keine Deutsche?)“


...



# RATIBA YAKO

<i>Tarehe - Datum</i>	<i>Shughuli - Programm</i>	<i>Maelezo - Notizen</i>
1)		
2)		
3)		
4)		
5)		
6)		
7)		
8)		
9)		
10)		
11)		
12)		

# DEIN PROGRAMM



13)		
14)		
15)		
16)		
17)		
18)		
19)		
20)		
21)		
22)		



# ANWANI NA SIMU

<i>Jina - Name</i>	<i>Anwani - Adresse</i>	<i>Simu &amp; Barua pepe - Handynummer &amp; E-Mail</i>
		! @
		! @
		! @
		! @
		! @
		! @
		! @
		! @
		! @
		! @
		! @
		! @
		! @
		! @
		! @



# KONTAKTE



		┌ @
		┌ @
		┌ @
		┌ @
		┌ @
		┌ @
		┌ @
		┌ @
		┌ @
		┌ @
		┌ @
		┌ @



# MAMBO YAKO - NOTIZEN

---



